KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO UNIONI YA KUSINI MWA TANZANIA

CHAMA CHA WACHUNGAJI/HUDUMA ZA MAOMBI

SIKU 100 ZA MAOMBI: MACHI 27 – JULAI 04, 2020

MADA: KUMWITA YESU KATIKA HITAJI LETU LA HARAKA

Limeandaliwa na: Melody Mason – Mratibu wa Maombi Kunferensi Kuu

Mtafsiri: Mch. Herbert I. Nziku – Mratibu - Huduma za Maombi: STUM

Juma la Kumi, May 29 – June 4, 2020

“UZURI KATIKA KUVUNJIKA”

Sitasahau, miaka kadhaa iliyopita, nilipokuwa najiandaa kuongoza huduma ya maombi katika tukio kubwa, jinsi Roho Mtakatifu alivyonitia hatiani juu ya jambo fulani mahsusi maishani mwangu ambalo nilihitaji kuliweka sawa na Mungu. Usiku ule, nikiwa nimezidiwa, nilizama magotini mwangu sakafuni na kuomba, “Ee Bwana, tafadhali nisamehe...”

Hata hivyo, ingawa niliungama dhambi yangu kwa Mungu, hatua fulani zilikuwa ni za muhimu ili kufanya marekebisho yanayofaa. Lakini sikuchukua hatua hizo mapema, hivyo nilikuwa sina hakika nini cha kufanya. Je! Ningeendelea na majukumu ya huduma ya maombi au ningempata mtu mwingine ili afanye badala yangu hadi niweke mambo sawa?

Kama kiongozi mwenye kuheshimika katika huduma, lilikuwa ni jambo linalodhalilisha kukubali mbele ya wengine kwamba nilimkosea Mungu katika eneo mahsusi. Sikutaka kutibua mambo na kuonekana dhaifu kiroho mbele ya wanatimu wenzangu, au kwa wageni wengi waliokuwa wakihudhuria mikutano ile. Kwa hiyo, nilikwenda kulala usiku ule, nikiwa na moyo mzito na machozi katika macho yangu, nikiwa nimeazimu kuwa nitamwomba mtu fulani mwingine aongoze huduma ya maombi siku iliyofuata.

Hata hivyo, asubuhi iliyofuata, nilipokuwa naanza kumtafuta mtu wa kushika nafasi yangu, Mungu alinizuia kadiri Roho Mtakatifu alivyoanza kuzungumza moyoni mwangu. “Melody, unatakiwa kuongoza huduma ya maombi asubuhi ya leo. Usimtafute mtu mwingine wa kufanya badala yako!” Huku machozi mapya yakitoka machoni mwangu nilisema, “Subiri Mungu... Humaanishi hili!” Lakini Roho Mtakatifu aliendelea kuzungumza na moyo wangu.

“Ndio, ninataka uongoze, hata hivyo, hutaongoza huduma hiyo kama *mtu yule unayetaka kila mmoja afikiri kuwa uko hiyo.* Hulioni hilo? Sitafuti watu wa kuongoza wanaoficha dhambi zao na kuenenda kana kwamba kila kitu kiko sawa. Ninatafuta *vyombo vilivyojitoa na kuvunjika*; vyombo vitakavyojinyenyekesha hadi kufikia kiwango cha kiburi kutoweka. Hapo tu ndipo nitakapovitumia kwa utukufu wangu. Ninajua kwamba hili ninaumiza, lakini unatakiwa kuliambia kusanyiko jambo nililokutia hatiani usiku uliopita. Uwe mwaminifu kuhusu namna ulivyonikosea! Kisha waalike mje *pamoja na wewe* msalabani kuziondoa dhambi zote na kufanya mapatano. Unaona, ikiwa watu wanasubiri hadi mambo yote yawe sawa ndipo waje, hawatakuja.”

Nilianza kukataa tena. “Siwezi kufanya hili, Bwana! Kila mmoja atanifikiriaje atakapoona jinsi nilivyokukosea?”

Roho Mtakatifu alizungumza na moyo wangu kwa upole huku akinitazamisha macho yangu kuelekea mbinguni. “Haijalishi wanachofikiri. Hili halihusu kulinda hadhi yako. Hili linahusu kumpa Mungu utukufu. Lakini, ili atende, ni lazima ujinyenyekeshe.”

Loh, asubuhi ile, sikutaka kabisa kutii msukumo wa Roho Mtakatifu. Kama ningekuwa na uwezo wa kukimbia kama Yona, au kujificha pangoni, ningeweza kulifanya hilo mara moja. Lakini nilijua ni kitu gani nilicholazimika kufanya. Nilitakiwa kutii.

Huku nikitetemeka na macho yangu yakiwa yamejaa machozi, nilikwenda mbele ya mamia ya watu asubuhi ile na kuwaambia lile Mungu aliloutwika moyo wangu. Ungeweza kusikia sindano ikianguka chini kwa jinsi chumba kilivyotulia huku watu wakisikiliza. “Yesu anatwambia tuje kama tulivyo” Niliyasema hayo kwa upole, huku nikiendelea kufuta machozi katika macho yangu. “Kwa hiyo, ninakuja kama nilivyo na ninawaalika nyinyi kuungana nami chini ya msalaba.”

Kwa mguso huo kila mmoja aliondoka kitini pake na kuja mbele ya chumba. Kulikuwa na vilio vya chini chini hapa na pale wakati watu mbali mbali wakiomba msamaha kwa Mungu kwa maeneo ya dhambi na mapatano yaliyokuwa yameingia maishani mwao. Na Roho Mtakatifu alikuwa pale. Katika kitabu cha Steps to Christ (Njia Salama) tunaambiwa:

> “Ukiiona hali yako ya dhambi, usisubiri kuyatengeza vizuri mambo yako wewe mwenyewe. Ni watu wengi kiasi gani wanaodhani kwamba sio wema kiasi cha kutosha kwenda kwa Kristo. Je! Unatarajia kuwa bora kwa juhudi zako mwenyewe?
> ‘Je! Mkushi aweza kuibadili ngozi yake, au chui madoa-doa yake? Kama aweza, ndipo na ninyi mwaweza kutenda mema, ninyi mliozoea kutenda mabaya’ *Yeremia 13:23.* Kuna msaada kwa ajili yetu katika Mungu pekee. Haitupasi kusubiri ushawishi wenye nguvu, fursa bora, au hasira takatifu. Peke yetu hatuwezi kufanya neno lo lote. Inatupasa kwenda kwa Yesu kama tulivyo.” (Steps to Christ, p. 31)

Kwa mtazamo wa ndani, ninathani hii ilikuwa moja ya huduma ya maombi tamu zaidi, nilizowahi kupitia, kwani Mungu alifanya kazi ya kina ya utakaso miongoni mwetu asubuhi ile. Mioyo mingi ilivunjwa vunjwa, lakini kulikuwa na uzuri kiasi gani na uponyaji katika kuvunjika. Katika Zaburi 51:17 Biblia inatwambia, “Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau.”

Ni dhabihu gani unayotafuta kumpelekea Mungu siku hizi? Je! Ni kazi zako bora, maombi yako bora, majaribio yako bora ya kuwa shahidi mwenye nguvu hata katikati ya matukio ya maisha yanayovunjika? Dhabihu zetu bora hazina uhusiano kwa lo lote na kazi zetu, bali ni hali ya kuvunjika kikamilifu kwa nafsi, kiburi na utoshelevu wote wa nafsi tunapokwenda chini ya msalaba. Kama usemavyo ule wimbo maarufu wa kitabuni *Mwamba Wenye Imara,* “Sina cha Mkononi, Naja Msalabani.” Hebu tuung’ang’anie msalaba leo!

MASWALI YA MOYONI:
Mungu hukaa wapi (angalia Isaya 57:15) na matokeo ya kuhuzunishwa kwa jinsi ya Mungu ni nini (angalia 2 Kor. 7:9-11)? Daudi aliomba nini katika ombi lake la toba (angalia Zaburi 51:1-19)? Pambanisha hili na jinsi Sauli alivyoitikia alipokemewa kwa ajili ya dhambi zake (angalia 1Sam. 15:1-30) Unapokuwa umeoneshwa dhambi zako, huwa unajifananisha na mhusika gani wa Biblia – yule anayetafuta kujihesabia haki na kudumisha heshima mbele ya watu, au yule anayekubali dhambi yake wazi wazi akiwa na moyo uliovunjika wa toba ya kweli?

CHANGAMOTO HAI MOYONI:

Unapopitia changamoto hii ya moyoni, mwulize Mungu endapo kuna kiburi cho chote katika maisha yako ambacho bado hujakisalimisha, au kama kuna mtu fulani katika eneo lako la ushawishi (familia, marafiki, wafanyakazi wenzako) unayetakiwa kumwomba msamaha. Kisha tii uongozi wa Roho Mtakatifu. (Zab.66:18, Mathayo 5:23-24, Mithali 28:13, Mathayo 6:14-15)

> "... hata kama kosa hili au lile litaonekana dogo kiasi gani katika macho ya wanadamu, hakuna dhambi iliyo ndogo machoni pa Mungu. Hukumu ya mwanadamu ina upendeleo, sio kamilifu; lakini Mungu huyapima mambo yote kama yalivyo. Mlevi anapuuzwa na kuambiwa kuwa dhambi yake itamwondoa asiende mbinguni; wakati kiburi, ubinafsi, na tamaa mara nyingi havikemewi. Lakini hizi ni dhambi ambazo kwa namna ya pekee zinamwudhi Mungu; maana zipo kinyume na wema wa tabia yake. Yule anayeanguka katika baadhi ya dhambi za jumla/kubwa anaweza kujisikia aibu na umaskini na hitaji lake la neema ya Kristo na baraka zisizo na kikomo alizokuja kuzileta." Steps to Christ, p, 30 (Njia Salama).

Siku ya 64, Ijumaa, Mei 29, 2020

TAARIFA ZA SIFA:

- Marlynn W., anasema "Tunamsifu Bwana kwani wakati huu wa Siku 100 za Maombi kwa ajili ya hili janga Mungu ametupatia kazi, chakula, na malazi. Bwana pia ametugusa ili kuhamia nje ya mji. Zaidi ya hayo, amenipatia fursa ya kuishuhudia jamii ya Kiislamu."
- Moses M., anasema "Tunawashukuru kwa kutuombea. Mungu amesikia maombi yenu! Inashangaza! Katika kipindi cha zuio la kitaifa nchini Namibia, karibia watu 1100 walijiandikisha katika masomo ya kujifunza Biblia, 70% kati yao sio Waadventista wa Sabato."

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** wanafunzi kote duniani ambao hawawezi kufanya kazi zao kwa sababu wamezuiliwa. Waombee ili Mungu awapatie fedha za kulipia masomo yao.
- **Ombea** wahanga wa vitendo vya ukatili majumbani kote ulimwenguni.
- **Ombea** familia ya Alexander Ostankin, mchungaji aliyeuawa akiwa kwenye huduma. Omba kwamba Mungu ageuze damu ya mfia-dini huyu ili iwe mbegu ya injili.
- **Ombea** wale ambao kwa sasa wanapambana na Covid-19. Ombea uponyaji wao kamili.

Siku ya 65, Jumamosi, Mei 30, 2020

WALETA AMANI WA MUNGU

*"*Heri wapatanishi; Maana hao wataitwa wana wa Mungu*."* – Mathayo 5:9

"Kristo ni 'Mfalme wa Amani' (Isaya 9:6), *na ni utume wake kurejesha amani iliyopotea kwa sababu ya dhambi duniani na mbinguni. '*Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo*.' Warumi* 5:1. *Ye yote anayepambana kuikataa dhambi na kufungua moyo wake kwa ajili ya upendo wa Kristo, anakuwa mshiriki wa amani hii ya mbinguni."* – Thoughts from the Mount of Blessing, p. 27

MASWALI YA MOYONI:
Wokovu katika Yesu hutupatia amani kamilifu. Lakini Yesu hakuiti tu ili uwe na amani pamoja kwa njia ya kuyasalimisha maisha yako kwake. Hapana, anakuita pia ili uwe wakala wa amani – *mleta amani*. Katika wakati huu wa zahama, utachagua kuwa wakala wa amani? Utafanya kila uwezalo ili kuangaza amani ya Mungu – uwepo wa upendo wake – katika maisha ya wale wanaokuzunguka wakiishi maisha yaliyojaa wasiwasi na hofu? Kama ulikuwa chanzo cha fujo na ugomvi katika familia yako au kanisa lako, utatafuta msamaha na kueneza amani ya Mungu?

TAARIFA ZA SIFA:

- Julius S., anasema "Kwa sababu ya hili janga Kanisa la Waadventista nchini Sierra Leone linarusha huduma zake katika Televisheni ya Taifa!"
- Cedrick B., anasema "Nilikuwa naombea uamsho wangu binafsi. Mungu amejibu ombi langu ndani ya Siku 100 za Maombi."

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** huduma ya Chuo Kikuu cha Kiadventista Colombia wakiendelea kutoa fursa za shughuli kwa wahamiaji toka nchini Venezuela. Omba kwamba familia nyingi zaidi, kule na mahali pengine ziweze kupata misaada.
- **Ombea** uinjilisti kwa njia ya redio ulioanza jijini Tokyo mwaka 2017. Mwombe Mungu aendelee kufungua milango kwa ajili ya matangazo ya redio ya Kianventista ili yaendelee kuwafikia watu wa Tokyo.
- **Ombea** msukumo wa "Utume Kwenye Miji - Spokane" unaotafuta kuongeza vituo vya mvuto mijini na kupata njia nyingi zaidi za humuma mijini ili kuwaokoa watu wa Spokane, Washington, Marekani.
- **Ombea** eneo la Rwenzori nchini Uganda, lililokumbwa na mafuriko mara nyingi katika majuma machache yaliyopita.

Siku ya 66, Jumapili, Mei 31, 2020

FURSA YA MATESO

*"*Heri wenye kuudhiwa kwa ajili ya haki; Maana ufalme wa mbinguni ni wao.*"* – Mathayo 5:10

"Yesu hawapatii wafuasi wake tumaini la kupata utukufu na utajiri wa kidunia, na wa kuwa na maisha yasiyo na majaribio, bali anawasilisha kwao fursa ya kutembea pamoja na Mwalimu wao katika njia za kujikana nafsi na aibu, kwa sababu ulimwengu hauwatambui.."
– Thoughts from the Mount of Blessing, p. 29

MASWALI YA MOYONI:
Upendo usio na ubinafsi, haki, utakatifu, na ukweli unapodhihirishwa na Wakristo waaminifu, Shetani atainua upinzani na chuki miongoni mwa wale wanaochagua kuipuuza sauti ya Roho Mtakatifu. Tunaweza kuwa na uhakikisho kuwa katika mateso yote tutakayokabiliwa nayo, Yesu atakuwa pamoja nasi na atajitukuza mwenyewe kupitia maisha yetu ya changamoto. Je! Umewahi kupitia mateso kwa sababu ya imani yako kwa Yesu? Kwa nini, au kwa nini hujawahi kupitia? Je! Utachagua leo kutupa kando shauku yo yote ya kuufurahisha ulimwengu, na kwa maombi ukalenga katika kudhihirisha utukufu wa Mungu, hata kama hilo litasababisha mateso?

TAARIFA ZA SIFA:

- Makanisa mengi yanazidi kuwa na ubunifu katika kuendesha huduma za Sabato washiriki wakiwa mbali kimwili.
- Janga hili limeuweka mbele umuhimu wa ujumbe wetu wa afya kwa washiriki wetu duniani kote. Shauku juu ya kinga ya kiafya NEWSTART (Kanuni 8 za asili za kiafya), inazidi kuongezeka. Sasa ni wakati mzuri wa kuwaongoza watu katika uelewa mpana wa sheria za Mungu za afya na uzima.

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** huduma ya Kanisa la Kiadventista kongwe zaidi nchini Norway, ambapo sasa linaongeza kituo cha mvuto cha kufundisha bure lugha ya Ki-Norway kwa wageni, shule ya upishi, mgahawa wa maongezi na zaidi ya hayo.

- **Ombea** huduma inayotembea ya afya kwa kutumia magari mawili mapya kule Chiapas, nchini Mexico. Ombea wagonjwa wanaowasafirisha na vikosi ya wahudumu wa afya vya mwisho wa juma wanavyovisaidia, kuwezeka uchunguzi wa afya wa bure, upasuaji mdogo, michakato ya afya ya kinywa, vipimo vya Utrasound, vipimo vya macho na mengine zaidi.
- **Ombea** uamsho wa uchaji wa kweli na shauku mpya ya uinjilisti ndani ya kila mshiriki ulimwenguni kote.
- **Ombea** kanisa nchini Burundi. Linapitia mapambano na masuala kadhaa wakati huu. Ni uingiliaji kati wa Mungu tu unaoweza kuleta amani.

Siku ya 67, Jumatatu, Juni 01, 2020

KUUDHIWA KWA AJILI YA UKWELI

*"*Heri ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu. Furahini, na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla*."* – Mathayo5:11-12

"Katika kila kizazi wajumbe wa waliochaguliwa na Mungu wamekuwa wakiudhiwa na kuteswa, na bado kupitia mateso yao uelewa kuhusu Mungu umekuwa ukisambaa nchi za mbali. Kila mwanafunzi wa Kristo inampasa kuingia kwenye mstari na kuendeleza kazi hio hiyo, wakijua kuwa maadui wa kazi hawawezi kufanya neno lo lote dhidi ya ukweli, bali wataukubali ukweli. Mungu anakusudia kuwa ukweli upelekwe mbele na kuwa somo la uchunguzi na mjadala, hata kama dharau itawekwa juu yake. Mioyo ya watu ni lazima itibuliwe; kila pambano, kila lawama, kila jitihada ya kudhibiti dhamiri, ni njia za Mungu za kuamsha mioyo ambayo kama si hivyo ingelala." – Thoughts from the Mount of Blessing, p. 33

MASWALI YA MOYONI:
Mateso yanapokuja, wakati sifa yako inapotukanwa, wakati maisha yako yanapokuwa hatarini, ndipo upendo wa Yesu utakapong'aa kwa mwangaza mkubwa zaidi. Jinsi unavyoitikia, kile unachosema, kila unachofanya unapokabiliwa na mashinikizo haya, kwa sehemu kubwa kitaamua nguvu ya uaminifu wako inavyoweza kuwa kwa wale wanaotafuta kuharibu maisha yako. Kwa nini usimwombe Yesu akusaidie kuwa mwaminifu na mwenye upendo leo na kila siku ili uweze kuonesha upendo kama huo hata ukiwa chini ya mateso? Je! Utamwomba hata sasa na ili akufanye kuwa Mkristo wa kweli atakayesimama kwa ajili ya Yesu hata kama dunia itaanguka?

TAARIFA YA SIFA:

- Wachungaji, wafanyakazi wa kanisa, na misukumo ya uinjilisti inachechemea kifedha kutokana na kupungua kwa zaka na sadaka. Lakini wanaweka matumaini yao kwa Mungu wa miujiza. Mungu anafungua milango mingi kwa ajili ya kuwahudumia watu wenye rasilimali chache kuliko ilivyokuwa hapo kabla.

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** jiko la supu linalotembea (kwenye gari), huduma inayotolewa na Kanisa la Waadventista wa Sabato Warwick, jijini Sydney, katika nchi ya Australia. Gari hilo linatoa huduma ya supu kwa watu wanaoishi pekee yao katika maeneo yao. Ombea Mungu awasaidie kujenga mwunganiko na jamii.
- **Ombea** shule mpya ya uganga kwa ajili ya Afrika Mashariki iliyopo Kigali, nchini Rwanda. Ombea wanafunzi wanaohitimu pale na watu wanaowahudunia.
- **Ombea** ujenzi mpya wa kanisa la chuo cha South Philippine Adventist ambalo liliharibiwa na tetemeko mwezi Disemba 2019.
- **Ombea** kituo cha mvuto kilichoko miongoni mwa Waislamu katika mji ambao haukutajwa. Baadhi ya Waislamu wameomba kuombewa wakati huu wa janga la Covid-19. Wanaamini kuwa maombi ya Waadventista yanasikiwa na Mungu.

Siku ya 68, Jumanne, Juni 02, 2020

LADHA YA YESU

*"*Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu.*"* – Mathayo 5:13

". . .Mungu anapowaita watoto wake kuwa ni chumvi, anawafundisha kuwa lengo la kuwafanya walengwa wa neema yake ni ili wawe mawakala katika kuwaokoa wengine... Chumvi ni lazima ichanganyike na kitu ilimowekwa; ili iweze kuhifadhi ni lazima ipenye na kuingia. Ndivyo kuwasiliana kwa mtu na mtu na kujishirikisha kunavyosaidia watu kufikiwa na nguvu inayookoa ya injili. Hawaokolewi kama umati, bali kama mtu mmoja mmoja. Mvuto wa mtu kwa mtu ni nguvu. Inatupasa tuwakaribie wale tunaotamani wanufaike. Ladha ya chumvi inawakilisha nguvu ya uzima ya Mkristo — upendo wa Yesu moyoni, haki ya Kristo ikiyajaza maisha. Upendo wa Yesu ni wenye kuenea na una nguvu. Kama unakaa ndani yetu, utamwagikia nje kwa wengine." – Thoughts from the Mount of Blessing, pp. 35-36

MASWALI YA MOYONI:

Kazi ya kumshuhudia Kristo ni wajibu wa kila mwumini. Kutumia mvuto binafsi kuelekeza kwa Yesu, kushiriki na wengine kile alichokufanyia, na namna alivyo njia, kweli na uzima, huu ndio wito wa maisha ya Ukristo. Je! Maishani mwako, unao marafiki au wafanyakazi wenzako wasioamini? Ama umejifungia mwenyewe kwenye "Kiputo cha Uadventista?" Kuna mtu angalau mmoja asiye Mkristo maishani mwako anayepata ladha ya Yesu kwa kutumia muda pamoja na wewe?" Mwombe Yesu leo akufanye kuwa chumvi yenye ladha nzuri kwa dunia!

TAARIFA YA SIFA:

- Matokeo ya mwanzo ya chanjo dhidi ya coronavirus inaonesha kuwa waliochanjwa waliongeza kinga dhihi ya kirusi. Tumsifu Mungu kwa ajili ya hatua hii kubwa kuelekea tiba kwa njia ya uwezo wa mfumo wa mwili kutengeneza kinga.

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** huduma ya kituo cha wakimbizi na wahamiaji kinachoendeshwa na Waadventista kule Manaus, nchini Brazil. Wanawahudumia watu toka Venezuela wanaoishi kama wahamiaji nchini Brazil. Omba Mungu abariki na kuzidisha njia za kiubunifu za kuwafikia watu.
- **Omba** Mungu awalete wageni sahihi katika duka la vyakula vya kiafya na mgahawa uitwao "Lentil" katika mji wa Yoshkar-Ola, nchini Russia. Mwombe Mungu abariki elimu ya upishi inayotolewa bure na njia nyinginezo za kuwafikia watu.
- Ombea washiriki na wanafunzi wa Kanisa na shule kule Guinobatan, Ufilipino. Shule ya kanisa imeharibiwa na kimbunga kilichotokea hivi karibuni. Ombea wote walioathirika kutokana na majanga mbali mbali ya asili ulimwenguni kote.
- **Ombea** kituo kiitwacho Shalem Lifestyle Center, kule Bogor, West Java. Kimekuwa kikipokea wageni wachache tangu janga la Covid-19 lilipoanza na kinachehemea kifedha. Waombee anapoendelea kutumia mtandao wa Zoom kuendesha semina za afya ili watu wengi waweze kufikiwa wakati huu wa zahama.

Siku ya 69, Jumatano, Juni 03, 2020

ANGAZA NURU YAKE

*"*Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*"* – Mathayo 5:14-16

"Ubinadabu ndani yake wenyewe hauna nuru. Nje ya Kristo tunafanana na mtafutaji asiye na taa . . . Lakini tunapoligeukia Jua la haki, tunapokutana na Kristo, nafsi yote inaangaza kwa mng'ao wa uwepo wake wa kiungu. Wafuasi wa Kristo inawapasa kuwa zaidi ya nuru katikati ya wanadamu. Wao ni nuru ya ulimwengu ...Malaika wa utukufu wanasubiri kuwasilisha kupitia ninyi nguvu ya mbinguni kwa roho zilizokaribu kupotea." – Thoughts from the Mount of Blessing, p. 40

MASWALI YA MOYONI:
Je! Uliisoma dondoo ya hapo juu? Unatambua kuwa malaika wanasubiri kutenda kupitia kwako ili kuwafikia watu waliopotea? Hili halishangazi? Umealikwa sio tu kujazwa na Roho Mtakatifu kwa ajili ya kutakaswa kwako binafsi, bali kushiriki kwa nguvu katika kuangaza ukweli, upendo, na haki ya Yesu kwa ulimwengu ambao muda wake unakwisha. Fikiria familia yako, rafiki zako, majirani zako, wafanyakazi wenzako. Mwombe Mungu akuoneshe ni nani anayehitaji nuru ya Yesu maishani mwake? Ni nani utakayemwombea na kuwasiliana naye juma hili?

TAARIFA ZA SIFA:

- Nchi nyingi ulimwenguni kote zimeanza kuondoa mazuio kwa uangalifu.
- Shirika la Afya Duniani linasema: "Kama kuna jambo ambalo kirusi hiki kinatufundisha, ni unyenyekevu." Watu wanajitambua jinsi walivyo dhaifu. Hii ni fursa kwa kanisa kuwaonesha watafutaji wa ukweli tumaini tulilonalo katika Yesu!

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Omba** baraka kwa ajili ya washiriki wanaoendesha biashara ya teksi kule Panama City, akiwatumia kama vituo vya mvuto vinavyotembea. Nusu ya raia wa Panama wanaishi Panama City.
- **Ombea** kituo cha mvuto cha Battambang, Cambodia. Kinajumuisha huduma ya mazoezi ya viungo, mgahawa wa vyakula vya mboga, kiwanja cha michezo, jengo la ibada, elimu ya afya, elimu ya muziki, na shule ya lugha. Omba baraka za Mungu kwa ajili ya mbinu hii yenye njia nyingi, na omba ili akuze huduma hii na awalete watu ambao amekuwa akiandaa mioyo yao.
- **Ombea** mkutano wa injili ujao wa vikosi vidogo vidogo chini ya Idara ya Huduma za Wanawake katika Unioni ya Magharibi mwa Nigeria.
- **Ombea** huduma ya kituo cha Kiadventista cha uponyaji wa waraibu kule Orlando, Florida, Marekani, kinachosaidia kupambana na madawa aina ya opioid. Ombea mamilioni ya watu wanaotafuta kuwa huru dhidi ya uraibu.

Siku ya 70, Alhamisi, Juni 04, 2020

SHERIA YA UPENDO

*"*Msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua torati au manabii; la, sikuja kutangua, bali kutimiliza. Kwa maana, amin, nawaambia, Mpaka mbingu na nchi zitakapoondoka,yodi moja wala nukta moja ya torati haitaoondoka ,hata yote yatimie.*"* – Mathayo 5:17-18

"Uzuri wa kiungu wa tabia ya Kristo, ambao walio bora sana na waungwana sana miongoni mwa wanadamu ni nuru hafifu tu; ... Yesu, ambaye ni chapa ya nafsi ya Baba, mng'ao wa utukufu wake; Mkombozi mwenye kujikana nafsi, katika safari yake yote ya upendo duniani, alikuwa ni mwakilishi hai wa tabia ya sheria ya Mungu. Katika maisha yake imedhihirika kwamba upendo wa mbinguni, kanuni za kufanana na Kristo, ni msingi wa sheria za unyofu wa milele." – Thoughts from the Mount of Blessing, p. 49

MASWALI YA MOYONI:
Sheria ya Mungu ni sheria ya upendo. Yesu alidhihirisha jinsi kushika sheria kulivyo kwa hakika. Unaweza kushika sheria kwa kutegemea kikamilifu msaada wa Roho Mtakatifu. Unapoamini kuwa atakusaidia kuishi maisha ya upendo usio na ubinafsi, na kwa imani, unapotenda matendo ya upendo, uweza wake wa uungu utakuwezesha na kutenda ndani yako kutaka na kutenda kulingana na mapenzi yake. Kama unachechemea katika uaminifu kwa sheria ya Mungu, unaweza kumwomba Yesu leo akusamehe, na kukujaza Roho Mtakatifu? Unaweza kumwomba akusaidie sio tu kushika sheria iliyoandikwa, bali roho ya sheria, ambayo ni upendo usio na ubinafsi na wa kujitoa kafara kwa Mungu na kwa watu wote?

TAARIFA ZA SIFA:

- Marietta A., anasema "Tunashukuru kwa maombi yenu! Kijana wangu wa kiume amepona ugonjwa wa Covid-19 na amerudia afya ya kawaida. Mungu Asifiwe
- Idadi ya vifo vya janga la Covid-19 nchini Hispania imepungua kiasi kikubwa kutoka 11% hadi 2% tu kwa sasa.

MAMBO YA KUOMBEA:

- **Ombea** kituo cha mvuto kilichopo Guatemala City ambacho hutoa huduma ya chakula, miswaki, bafu, na sehemu ya kufua nguo kwa wale wanaoishi mitaani. Tafadhali mwombe Mungu akidhi mahitaji ya kina ya wageni wanaotembelea kituo kile, na kuwasaidia wapate tumaini kwa ajili ya umilele.
- **Ombea** vyombo vya habari vilivyojitoa kutoa habari mpya kuhusiana na janga la Covid-19. Omba kwamba Mungu awasaidie kuwasiliana kwa umakini unaofaa.
- **Ombea** wale wanaokabiliana na wasi wasi, msongo, na hofu wakati wa zahama hii. Waombee waweze kupata msaada, kutiwa moyo, tumaini na uponyaji katika Yesu.
- **Ombea** wachungaji, walimu, wamishonari, na washiriki katika nchi ya Laos (nchi iliyo Kusini Mashariki mwa Asia). Baadhi ya maeneo ni vigumu kuyafikia kwa njia ya teknolojia ili kutoa huduma wakati huu wa hili janga na utembeleaji wa mtu mmoja mmoja ni wa muhimu ili kuwafikia watu wanaohangaika kwa masuala mbali mbali.